UTANGULIZI

Ukisoma simulizi, tafiti na machapisho mbalimbali kutoka kwa waandishi wa nyakati tofautitofauti tangu kuumbwa kwa ulimwengu utakutana na maelezo na michango ya watu mbalimbali waliomwelezea mwanamke kama kiumbe dhaifu asiyeweza kufanya  jambo lolote linalohitaji nguvu na kufikiri kwa umakini katika jamii. Wapo pia waliojikita kumtafiti mwanamke na kutoa maoni yao kuhusu nguvu kubwa aliyo nayo mwanamke katika utendaji wake.

Imethibitishwa kuwa mwanamke akiitumia nguvu yake vizuri basi anaweza kufanya makubwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha jamii inaishi maisha yenye furaha na amani. Mimi nami kama mwanamke nimetia bidii kumwangalia na kujifunza kuhusu mwanamke tangu kuzaliwa kwake, kukua na utendaji wake kwenye jamii. Nami nimeona ni vema nikatoa mchango wangu katika kumwelezea mwanamke nguvu na uwezo alionao katika jamii.

Mwanamke ni kiumbe mwenye nguvu sana na kwa nguvu hiyo anaweza kusababisha matokeo chanya na hasi katika jamii, kutokana na namna atakavyoamua kuitumia nguvu iliyo ndani yake. Watu wengi (wanaume kwa wanawake) wameshindwa kufaidi matunda yanayotokana na nguvu iliyo ndani ya mwanamke, kwa sababu waliamini kwamba mwanamke hawezi kuwa na kitu cha tofauti cha kuifaa jamii. Wakati mwingine mwanamke mwenyewe anaweza akahangaika na maisha fulani yasiyo na mwelekeo, kwa sababu tu hajajitambua na kuiona nguvu kubwa aliyonayo ndani yake!

Nguvu kubwa iliyo ndani ya mwanamke ikitumiwa vizuri, huleta faida kubwa kwenye jamii na katika kitabu hiki tutaona na kujifunza nguvu kubwa aliyo nayo mwanamke na namna ya kuitumia ili kupata mafanikio makubwa katika maisha yetu.

Historia inaonyesha kwamba katika jamii za wanadamu ulimwenguni kote kwa asilimia kubwa zimemchukulia mwanamke kama kiumbe duni na dhaifu, kiumbe ambacho unaweza kukitendea ubaya kama upendavyo na kutendea wema kwa hisani.

Kwa bahati mbaya wanawake nao walikubaliana kuiona hali hiyo kama kitu cha kawaida kabisa. Ukisoma Biblia utaona maandiko yanaonyesha wanawake hawakutambuliwa kama ni watu, tawala zilipotakiwa kuhesabu watu wao waliwahesabu wanaume tu, wanawake hawakuhesabiwa.

Matayo 14:21Idadi ya watu waliokula, bila kuhesabu wanawake na watoto, ilikuwa kama wanaume elfu tano.NaMathayo 15:38

Hao waliokula walikuwa wanaume 4,000, bila kuhesabu wanawake na watoto.

Kwahiyo hapa tunaona kwa destuli za kiyahudi mwanamke hakuhesabiwa kama mtu, ndiyo maana idadi ya watu waliokula waliohesabiwa walikuwa wanaume watupu na maandiko yanakiri wazi kwamba wanawake hawakuhesabiwa. Najaribu kufikiri kwamba pengine hawakuwahesabu wanawake na watoto kuwa ni viumbe waliokula kwa sababu waliona hawana thamani ya utu. Au pengine hawakuwahesabu kwa sababu walikuwa wanakula kiasi kidogo cha chakula ndipo wakaona haina haja ya kuwahesabu kama wamepunguza chakula. Au kwa sababu walikuwa hawawezi kwenda vitani kupigana?

Kikubwa tunachokiona hapa ni kwamba mwanamke hakuwekwa kwenye hesabu ya watu waliokula. Sasa mwanamke wa wakati huo alijionaje? Kwa vyovyote alijiona mnyonge sana asiyekuwa na thamani kwenye jamii. Na hali hii ilipelekea kujengeka kwenye jamii kwamba, wazazi wanapopata mtoto wa kiume wanaona amezaliwa mtu, lakini anapozaliwa mtoto wa kike anaonekana kama ni kiumbe fulani dhaifu kimeongezeka kwenye familia.

Kwa Mfano katika nchi yetu ya Tanzani mwaka huu 2022 ni mwaka wa kuhesabiwa (SENSA) na serikali yetu imesisiza kila mtu ahesabiwe kwa ajili ya kutaka kujua idadi ya watu waliopo, na idadi hiyo ya watu itaisaidia serikali kuweka mipango ya maendeleo kulingana na idadi ya watu wake. Sasa fikiria waseme tunahesabu wanaume tu, wewe kama ni mwanamke utajisikiaje? Na je!

Utakuwa na hamu ya kuendelea kwenda kazini? Kama ni mwalimu au Daktari utaendelea kuhudumia watu kwa furaha? Chukulia sasa kwa Tanzania ambapo Rais wetu ni mwanamke, hapo maana yake raia namba moja ambaye ni rais wa nchi hawezi kuhesabiwa. Hali hii inapojitokeza kwenye jamii inasababisha kundi hilo lisilohesabiwa kujiona wanyonge wasio na faida katika jamii hiyo.

Ili kujikomboa na hali hii ya mfumo dume wanawake tumekuwa na majukwaa na kampeni mbalimbali za kutafuta haki sawa na mwanaume. Nachukua nafasi hii kuzipongeza juhudi hizo ambazo kwa kiasi fulani heshima ya mwanamke kuwa mtu inaonekana japo bado ile nguvu kubwa aliyo nayo mwanamke haijafanya kazi inavyostahili.

Ukitulia na kutazama kwa undani jambo hili huku ukilinganisha ukubwa wa nguvu ya mwanamke ilivyo, utaona kutafuta haki sawa kati ya mwanamke na mwanaume siyo suluhuhisho sahihi la kumkwamua mwanamke katika hali hiyo.

Suluhisho sahihi ni mwanamke kuitambua nafasi yake ambayo Mungu amempa katika jamii na namna Mungu alivyomthamini mwanamke tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mwanamke kutambua wajibu wake sahihi kwa mwanaume na mwanaume kutambua wajibu wake, thamani na nguvu iliyo ndani ya mwanamke. Lakini kwa ujumla jamii nzima duniani kote inahitaji itambue nafasi ya mwanamke, nguvu kubwa aliyo nayo katika kuifanya dunia iwe mahali pazuri pa kuishi na kufurahia maisha.

Karibu sana twende pamoja ninapokutazamisha nguvu ya mwanamke na mbinu za kufanya ili kila mmoja wetu aweze kupata mafanikio makubwa kutoka kwa mwanamke yeyote aliye karibu yako, awe ni bibi yako, mama yako, shangazi yako, dada yako, mke wako, rafiki yako, jirani yako, mfanyakazi mwenzako, mtoto wako, mjukuu wako na mtu yeyote wa jinsia ya kike utakayekutana naye uone namna ya kuvuna matunda kwake. Karibu tujifunze pamoja na Mungu akubariki sana.